USAFIRI

# Kilio na kicheko nauli mpya leo

**Na Elizabeth Zaya**

KUANZIA leo, utekelezaji nauli mpya za mabasi ya mijini na masafa marefu umeanza rasmi, ukiibua hisia mseto mitaani: furaha kwa wasafirishaji na majonzi kwa abiria wanaobeba mzigo wa gharama mpya za maisha.

Katika mazungumzo na wananchi jijini Dar es Salaam jana, wengi wa waliohojiwa na Nipashe walieleza kuwa ingawa wanaelewa sababu za kupanda kwa nauli, hasa ongezeko la gharama za mafuta duniani, hali hiyo imeongeza presha kubwa katika maisha yao ya kila siku.

Makero Lucas, mkazi wa Tegeta jijini Dar es Salaam, alisema wananchi hawapingi mabadiliko hayo kwa sasa, lakini wanaomba yawe ya muda tu.

"Tunajua sababu ya kupanda kwa nauli ni gharama za mafuta zilizochangiwa na hali ya kimataifa. Lakini tunaomba hali ikirejea kawaida, nauli nazo zishuke. Kwa sasa kila kitu kimepanda. Ukienda sokoni unaambiwa gharama ya usafirishaji imeongezeka," alisema.

Kwa wananchi wengi, kupanda kwa nauli siyo changamoto ya usafiri pekee bali ni mnyororo wa gharama unaogusa kila kitu, hasa chakula.

Agatha Mlinga, mkazi mwingine wa Jiji la Dar es Salaam, anasimulia jinsi mabadiliko hayo yalivyobadili bajeti ya familia yake.

"Nilikuwa nakwenda sokoni na Sh.10,000 inanitosha kununua chakula cha familia. Sasa haitoshi kabisa. Hata nyama imepanda bei. Tunaomba serikali itusaidie, hata kwa muda, ibebe mzigo wa mafuta ili sisi tusipate tabu hii yote," alisema.

> **"Si ongezeko kubwa sana, lakini lina msaada. Tulikuwa tunafanya kazi kwa presha kubwa, ukifikiria mafuta yamepanda lakini mapato ni yale yale. Sasa angalau tutapata nafuu kidogo,"**

Kwa mtazamo wake, suluhisho la haraka linaweza kuwa ni serikali kuweka ruzuku katika mafuta ili kupunguza athari kwa wananchi wa kawaida.

Katika upande mwingine, baadhi ya wafanyakazi wanasema kupanda kwa gharama za maisha hakujalingana na ongezeko la kipato.

Mfanyakazi mmoja wa serikali ambaye hakutaka kutajwa jina lake gazetini, alisema hali ya sasa inalazimu serikali kuangalia upya mishahara.

"Hakuna mtu ambaye hajalalamika kwa sasa. Gharama zinapanda kila siku lakini kipato hakiongezeki. Watu wengi tunaishi kwa msongo wa mawazo. Serikali ituangalie, hata kuongeza mishahara kidogo kutasaidia," alisema.

Aliongeza kuwa kuna haja pia ya kudhibiti wafanyabiashara wanaotumia fursa hiyo kupandisha bei kiholela.

Tofauti na abiria, baadhi ya madereva na makondakta wa daladala wamepokea mabadiliko hayo kwa mikono miwili, wakisema yamewapa ahueni baada ya muda mrefu wa kufanya kazi kwa hasara.

Dereva mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Noel, anayefanya safari kati ya Makumbusho na Bunju, jijini Dar es Salaam, alisema ongezeko hilo litawasaidia angalau kufikia malengo ya kila siku kwa wamiliki wa magari.

"Si ongezeko kubwa sana, lakini lina msaada. Tulikuwa tunafanya kazi kwa presha kubwa, ukifikiria mafuta yamepanda lakini mapato ni yale yale. Sasa angalau tutapata nafuu kidogo," alisema.

Kwa mujibu wa viwango vipya vilivyotangazwa Aprili 17 mwaka huu na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), nauli za daladala zimeongezeka kwa wastani wa Sh. 100 katika baadhi ya safari.

Safari iliyokuwa Sh. 600 sasa ni Sh. 700, Sh. 1,100 imekuwa Sh. 1,200, huku nyingine zikiongezeka kwa kiwango kinachofanana.

Hata hivyo, wanafunzi wameendelea kulindwa kwa kulipa Sh. 200 kama ilivyokuwa awali.

Kwa mabasi ya masafa marefu, nauli zimepangwa kulingana na umbali, daraja la basi na aina ya barabara, huku gharama kwa kilomita zikiongezeka kwa mabasi ya kawaida na ya kati.

Kwa upande wa teksi mtandao, safari za chini ya kilomita moja zitagharimu kati ya Sh. 4,000 hadi Sh. 5,000.

Kwa ujumla, hali ya sasa inaonesha mgawanyiko wa hisia: kicheko kwa wasafirishaji wanaopata nafuu, na kilio kwa abiria wanaobeba mzigo wa gharama mpya.




Daladala zikisubiri kupakia abiria jijini Dar es Salaam. Nauli mpya zilizotangazwa na LATRA Aprili 17 mwaka huu zimeanza kutumika leo.
**PICHA: MAKTABA**

Habarileo Ijumaa Mei 1, 2026 Pg 3

# Mwigulu: Bodaboda muhimu kwa uchumi

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba amesema pikipiki za magurudumu mawili 'bodaboda' ni muhimu katika uchumi.

Dk Mwigulu alisema hayo wakati akijibu swali la Mbunge wa Bukoba Mjini, Johnson Mutasingwa (CCM) bungeni Dodoma jana.

Mutasingwa alitaka kufahamu mpango wa serikali wa kuiwezesha sekta ya bodaboda iwe sekta rasmi itakayoweza kuchochea uchumi na kuwa ajira inayotambulika ili ikuze uchumi wa nchi.

Dk Mwigulu alisema bodaboda ni sekta rasmi inayotambulika na serikali na wanatambulika kama maofisa wasafirishaji.

"Ni rasmi kwa sababu ni sekta inayoajiri vijana wengi wa Kitanzania, inayotoa huduma ambayo inatambulika na kila Mtanzania, inawanufaisha Watanzania wote wa mijini na vijijini na ni sekta inayotumika katika sekta ya kiuchumi, kwa hiyo ni sekta ambayo ni kiungo muhimu katika uchumi," alisema Dk Mwigulu.

Alisema sekta hiyo inaandikishwa, iliyounganishwa kwenye taratibu za mitaji, kwa maana vijana wanaweza wakapata mikopo ya kuongeza mitaji katika sekta hiyo.

"Serikali inaitambua kama sekta rasmi inayochangia Pato la Taifa na utengenezaji wa ajira. Zamani ilikuwa wanaofanya kazi hizo ni vijana ambao walikuwepo tu mtaani lakini kwa sasa ni sekta inayofanywa na watu wote wenye elimu na wasio na elimu pamoja na wanawake na wanaume. Katika ahadi za siku 100 za Rais Samia Suluhu Hassan za kutoa mikopo kwa vijana, ni pamoja na vijana waliopo katika sekta hiyo," alifafanua.

Dk Mwigulu alitoa rai kwa ofisi za serikali na udhibiti wanapokutana na vijana hao watambue wanakutana na sekta muhimu inayochangia kutengeneza ajira, Pato la Taifa na kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja katika familia, hivyo vijana hao wanapohitaji kuwezeshwa wawezeshe na watambue kwamba serikali ipo pamoja nao katika kuhakikisha shughuli yao inakuwa sekta yenye ufanisi.

Aliahidi kuhakikisha kila eneo mjini na vijijini kadri wanavyopata ushauri wa wabunge kuendelea kuboresha mazingira ya vijana hao ili wafanye shughuli zao kwa ufanisi.

*Imeandikwa na Angela Semaya (Dodoma) na Rehema Lugono (Dar).*

CamScanner